UFUGAJI WA KUKU WA ASILI

SEHEMU YA KWANZA

RLDC
RURAL LIVELIHOOD DEVELOPMENT COMPANY

inter cooperation

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

swisscontact

RURAL LIVELIHOOD DEVELOPMENT COMPANY

RLDC na Uboreshaji wa Maisha Vijijini

Shirika la Rural Livelihood Development Company (RLDC ni moja ya mafanikio ya ushirikaiano kati ya Tanzania na Uswisi kwenye mchakato wa kupambana na umaskini na kuboresha maisha ya jamii za vijijini. Hii ni taasisi isiyo ya kibiashara ili yoanzishwa mwaka 2005 na mashirika ya Intercooperation na Swisscontact, lengo kuu likiwa kutekeleza Programu ya kuendeleza maisha ya jamii za vijijini (RLDP). Programu hii inasha bihiana na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupambana na Umaskini (MKUKUTA). Dhamira kuu ya RLDC ni Kuendeleza/kuboresha mifu mo ya masoko ili kuwawezesha wazalishaji wa vijijini kutumia
fursa zilipo kuboresha maisha yao.

Kwa sasa, RLDC inatelekeleza awamu ya pili ya mpango wake (2008-2011) na inaweka msukumo zaidi kwenye uendelezaji wa mifumo ya masoko. RLDC inafanya kazi katika mikoa sita ya Kanda ya kati-Dodoma, Singida, Morogoro, Shinyanga, Tabora, na Manyara. Jamii nyingi maskini zinaishi katika ukanda huu wenye sehemu kubwa yenye hali ya mvua chache na nusu jangwa inayostawisha shughuli chache za kiuchumi.

Hata hivyo kuna fursa nyingi sana zinazoweza kutoa ajira na kuboresha ya jamii zake. RLDC inafadhiliwa na Serikali ya Uswisi kupitia shirika la Uswisi la maendeleo (SDC).

Kwa sasa RLDC inawezesha sekta za pamba, alizeti, maziwa, ufugaji wa kuku wa kienyeji, mpunga na habari kupitia vipindi vya redio kwa ajili ya wazalishaji wa vijijini.

“RLDC inaboresha mifumo ya masoko ili kuwezesha wazalishaji wa vijijini kuinua maisha yao”

Sehemu ya Kwanza

Ufugaji wa kuku wa asili kwa 'Mfumo wa Bariadi'

1.0 Utangulizi

Mwaka 2008/9 RLDC ilifanya majaribio ya mfumo wa ufugaji wa kuku wa asili kupitia vikundi vidogo vya wafugaji wa vijijini katika vijiji vya Bupandagila na Mbiti, Wilayani Bariadi katika Mkoa wa Shinyanga. Huu ni ufugaji wa ushirika unaolenga kusaidia wazalishaji wadogo wa mazao ya kuku. Utaratibu huu unahusisha mgawanyo wa kazi katika ufugaji ili kurahisisha na kusaidiana majukumu na gharama.

Lengo kubwa la majaribio haya ilikuwa ni kuona kama mfugaji mmoja angepunguziwa majukumu yake katika uzalishaji ili kuongeza uwezo wake wa uzalishaji. Vijiji husika vilifanikiwa kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa kuku watano hadi kufikia kuku mia moja katika miezi michache. Mafanikio ya mradi huu ndio chachu iliyofanya RLDC kuona umuhimu wa kufundisha na kudurufu mfumo huu katika maeneo mengine ya nchi na kuweka wazi kwa watu wengine ambao watakuwa tayari kujihusisha na ufugaji wa kisasa na kibiashara wa kuku wa asili bila usaidizi wa wafadhili.

Mfumo huu unaonyesha nyenzo muhimu zinazolenga kurahisisha ufugaji wa kuku kwa wafugaji wadogo walioko vijijini kwa kupunguza majukumu ambayo mtu mmoja angetakiwa kufanya katika mlolongo wa uzalishaji. Mfumo unalenga katika utendaji wa vikundi vidogo vidogo vinavyopewa mafunzo kulingana na kazi waliyochagua kufanya katika mlolongo mzima wa uzalishaji. Ufugaji wa namna hii unamfanya mfugaji awe na sehemu ndogo anayoimudu katika mfumo mzima wa ufugaji kuku (mfano kikundi kimoja kujihusisha na utotoleshaji wa vifaranga pekee au utafutaji wa masoko). Mfumo huu pia umeazima baadhi ya mafanikio kutoka mfumo uliofanyiwa kazi huko Bangladesh na kufanikiwa katika nchi nyingi zikiwemo za Afrika ya Mashariki.

Licha ya ukweli kwamba mfumo huu unapunguza majukumu, pia unaongeza uwezekano wa wafugaji kupata huduma zingine muhimu wakiwa katika vikundi. Huduma hizo ni pamoja na mafunzo, mikopo, uwezekano wa kujifunza kwa pamoja ujuzi mpya katika ufugaji na hata kuwa na sauti ya pamoja katika soko. Katika kijitabu hiki utaelezwa zaidi jinsi ya kufanya kazi kupitia mfumo huu wa Bariadi.

2.0 ‘Mfumo wa Bariadi’

Mfumo huu wa uzalishaji huwaweka wazalishaji katika ushirika au kikundi kimoja kikubwa cha pamoja chenye taratibu, uongozi na maadili yake. Umoja huu wa wafugaji husajiliwa kisheria. Viongozi wa kikundi hiki (Kamati kuu ya utendaji ya kijiji) hutokana na viongozi wa vikundi vidogo vidogo vinavyoundwa na shughuli wanayoifanya katika uzalishaji (mfano wazalishaji wa chakula, wanaohusika na afya ya kuku n.k). Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti wa kikundi kidogo ndio wanaounda uongozi wa kikundi kikubwa (umoja wa wafugaji) cha hapo kijijini.

Mfumo huu wa uongozi unatakiwa kuzingatia uwakilishi mzuri wa vikundi vyote katika jamii husika ili kuleta uwiano wa utendaji na maamuzi yanayolenga maendeleo ya vikundi vyote kijijini. Pia mfumo huu unasaidia uratibu wa maendeleo katika sekta nzima.



Mfumo wa uongozi wa umoja wa wafuga kuku kijijini

Kutokana na mafanikio mazuri ya kiutendaji yaliyopatikana huko Baraidi, RLDC imeamua kushirikisha wadau wengine wa uzalishaji katika wilaya nyingine za Ukanda wa Kati ili kuendeleza biashara na sekta ya uzalishaji wa kuku wa asili. Hata hivyo, tumejifunza kuwa mfumo ungeweza kufanya vizuri zaidi kama yafuatayo yatazingatiwa.

A. Wafugaji wa kuku wote waliojiunga katika kikundi wawe na umoja wa wafugaji pale kijijini. Kwa maana ya kwamba sharti mojawapo la kuwepo katika kikundi ni kuwa mfugaji wa kuku wa asili. Kwa kuanzia, kila mmoja atafuga kuku wa umri wa mwezi mmoja hadi kufikia kuuzwa kwa wafanyabiashara. Wafanyabiashara, watengenezaji wa chakula, wauza madawa na watu wengine wote hawataruhusiwa kuwepo kwenye kikundi ila tu kama watafuga kuku.

B. Kila mtu katika umoja wa wafugaji wa kuku anapaswa kuwa katika kundi mojawapo maalumu katika uzalishaji. Hiyo inamaanisha kuwa kila mfugaji atakuwa na kazi mbili katika ufugaji; atafuga kuku hadi umri wa kuuza na atajihusiha na kikundi kidogo kimojawapo katika mzungukuko wa uzalishaji. Hii itampa nafasi ya kujifunza mambo mengi yahusuyo biashara ya kuku. Vikundi hivyo vimeganyika kulingana na majukumu kama invyooneshwa hapa:

    - Utotoleshaji wa vifaranga
    - Utunzaji wa vifaranga vya siku moja
    - Uboreshaji na utunzaji afya ya kuku
    - Utengenezaji wa chakula cha kuku
    - Utafutaji wa habari na Masoko ya kuku
    - Kuweka na kukopa

Makundi mawili ya mwanzo yaweza kuunganishwa kulingana na hali halisi ya wadau. Utengenezaji wa vikundi mbali mbali utajadiliwa katika mafunzo ya awali ya umoja wa wazalishaji. Pia hali halisi ya wazalishaji kijijini itajadiliwa kama kuwa na makundi yote (mawili ya mwanzo) ama kuwa na kundi moja tu katika hayo.

3.0 Shughuli za vikundi

3.1. Kikundi cha watotoleshaji vifaranga

Hiki kitakuwa na jukumu la kulea kuku wazazi wenye sifa inayopendwa na kikundi na wanaweza kuchanganya mbegu ili kupata kuku bora. Kwa kuanzia, kikundi kitatumia njia za asili za kutotolesha na baadaye kulingana na uhitaji kuongezeka waweza kuamua kutumia viatamizi. RLDC kupitia watendaji wake vijijini itakusanya habari muhimu kuhusu viatamizi na kuhakikisha habari hizi zinawafikia wahusika wa kikundi.

3.2 . Kikundi cha Walezi wa vifaranga

Hiki kinahusisha vifaranga wa siku moja hadi wiki tano. Wanakikundi watawajibika kuchukua vifaranga toka kwa watotoleshaji na kuvilea hadi kufikia umri tajwa. Wanakikundi watawajibika kuwapa chanjo na madawa muhimu kulingana na magonjwa yanayojulikana katika eneo husika. Wanachama wa kikundi hiki watahitajika kuwekeza katika chanjo na mahitaji mengine mengi yatakayohitajika kwa ajili ya afya bora ya kuku. Pia watahitajika kuwekeza katika mabanda mazuri yenye kutunza vifaranga mbali na maadui mbalimbali na uambukizo wa magonjwa. Baada ya wiki tano, vifaranga watauzwa kwa wanavikundi wengine watakaowatunza hadi umri wa kuuzwa au kutunzwa kama kuku wa mbegu. Hata hivyo, wakati wote wa utunzaji, wanachama watahitaji huduma toka kwa kundi linaloshughulika na afya ya kuku pamoja na watengenzaji wa chakula.

3.3. Kikundi kinachohusika na afya ya kuku.

Wanachama wa kikundi hiki watafundishwa namna bora ya kutambua magonjwa, kuchanja kuku na kutibu magonjwa mbalimbali ya kuku. Wanachama wa kundi hili watafanya kazi kwa karibu na wataalamu wa serikali waliopo katika eneo lao ili kuboresha huduma yao pale wanapoona wanahitaji utaalamu zaidi. Wanachama wa kikundi hiki watalazimika kuwekeza katika kununua madawa, chanjo na vifaa vya kutunza baridi.

Chombo cha asili cha kutunza joto – vifaranga

3.4. Kikundi cha watengenezaji chakula

Hiki kitahusika na kuchanganya chakula na kusaga kulingana na mahitaji yaliyopo. Kikundi kitazingatia aina ya vyanzo vya vyakula vinavyopatikana katika maeneo yao. Chakula kinachochanganywa kitaalamu husaidia kupunguza muda wa kuku kufikia muda wa kuchinjwa. Wanachama wa kikundi hiki watahitajika kuwekeza katika kununua vifaa vya kusagia na kuchanganya chakula.

3.5. Kikundi cha masoko

Kikundi kitahusika na kutafuta habari za masoko ndani na nje ya kikundi na kuwaunganisha wafugaji na wanunuzi mbali mbali toka masoko mengine kwa bei nzuri. Wanachama wa kikundi hiki watahitajika kuwekeza katika gharama za usafiri kwa ajili ya kutafuta masoko.

3.6. Kikundi cha kuweka na kukopa.

Wanachama wake watasimamia shughuli zote za kuweka na kukopa kwa wanachama wote wa umoja katika kijiji husika. RLDC imekusudia kutumia na kufundisha wafugaji mfumo wa kuweka na kukopa unaotumiwa na shirika la Care International. RLDC haitatoa mtaji wowote ila kupitia mfumo huu, tunatarajia kwamba vikundi vitajiwekea malengo mahususi ya kuwafanya wanachama wote waweze kuweka ili wawe na nafasi ya kukopa hapo baade. Kikundi pia kitajiwekea taratibu mbalimbali za kuweka na kukopa ikiwa ni pamoja na viwango maalumu na vipindi vya kuweka, kuchukua mkopo na kurudisha na riba zake. Taratibu zote zitathibitihwa na kupitishwa na wanachama wote kabla hazijaanza kutumika.

Jedwali hapo chini linaeleza kwa kifupi kila kikundi, majukumu yake, ujuzi unaotakiwa (ambao kila kikundi kitafundishwa) pamoja na eneo la uwekezaji.

Jina la kikundi	Jukumu	Ujuzi unaohitajika	Eneo la kuwekeza
Watotoleshaji wa vifaranga	Kuku wazazi	Kuku wazazi bora Matunzo mahususi ya kuku Chakula na nyumba bora Magonjwa ya kuku	Kuku bora - wazazi
Watunzaji wa vifaranga	Kulea vifaranga	Magonjwa Nyumba za vifaranga Chakula cha vifaranga	Nyumba bora zenye joto mahususi Vifaa vya kulishia
Afya ya kuku	Afya ya kuku	Udhibiti wa magonjwa Mchanganyiko bora wa chakula Madawa na kinga Matumizi bora ya dawa na vyakula	Chanjo na madawa Sanduku la kutunzia dawa (Cold box)
Watengeza chakula	Utengenezaji wa chakula bora	Vyanzo bora vya vyakula Utengenezaji wa chakula Matumizi sahihi ya chakula kwa umri	Vyanzo vya vyakula Vifaa vya kuchanganyia na kusagia
Masoko	Habari za masoko	Utafutaji wa masoko Namna ya kupata habari za masoko	Gharama za usafiri na kupata habari za masoko
Kuweka na kukopa	Kuweka na kukopa	Namna ya kuweka kumbukukumbu za kuweka na kukopa	Kuweka na kukopa

4.0 Uongozi

Kama ilivyoelezwa hapo juu, kila kikundi kidogo kitachagua mwenyekiti na naibu mwenyekiti kutoka kwa wanachama wake. Umoja wa wafugaji kama kikundi kikuu cha wafugaji watachagua mwenyekiti na naibu katibu wake ambao hatakuwa na madaraka katika vikundi wanavyotoka. Viongozi wa vikundi (Mwenyekiti na naibu wake) watatengeneza kamati kuu ya uongozi wa ushirika na watakutana kadiri inavyohitajika na mujibu wa makubaliano ya mipango ya kikundi. Kamati ya utendaji itapokea taarifa toka kwa viongozi wa kila kikundi ni kitakuwa na maamuzi ya mwisho katika umoja. Kamati hii itakuwa na maauzi juu ya usafirishaji wa kuku ndani ya umoja. Pia kamati itafanya maamuzi juu ya bei za:

- Vifaranga wa siku moja
- Vifaranga wa wiki tano
- Dawa, chanjo na huduma zake
- Chakula cha kuku
- Changizo la huduma ya masoko ya pamoja
- Taratibu zote na riba za mikopo

Kumbuka kwamba; wanachama wa kila kikundi watafundishwa kulingana na mahitaji ya utendaji wao. Wanachama wote watapatiwa vitini vya kila somo wanalofundishwa kwa ajili ya kumbukumbu zao.

5.0 Mwisho

RLDC inatarajia kuwa mfumo huu utaleta manufaa makubwa kwa wafugaji wa kuku wa asili kwa kubadilisha mfumo holela wa ufugaji ili kupata kuku bora, wenye bei nzuri katika soko na idadi inayoweza kutegemewa kila wanapohitajika. Pia tunaamini kuwa mfumo wa masoko utaboreshwa kwani kila mtu atajishughulisha na jukumu moja analoweza kulimudu vizuri kwa muda muafaka. Ongezeko la kuku bora linatarajiwa kuongeza ulaji wa kuku mijini na vijijini na hivyo kuboreha afya za walaji kwa kupata protini nyingi zaidi. Hali hii inatarajiwa kuongeza kipato kwa wafugaji wa kuku wa vijijini na hivyo kuoboresha maisha yao. Serikali pia inatarajiwa kunufaika na mfumo huu kwani mapato kupitia kodi mbalimbali yataongezeka. RLDC inatamani kuona wadau wa kuku wa asili wanaweza kuuza kuku katika masoko makubwa ya ndani na nje ya nchi.

RURAL LIVELIHOOD
DEVELOPMENT COMPANY

Jengo la NBC
Ghorofa ya Pili, Mtaa wa Nyerere
S.L.P. 2978, Dodoma, Tanzania.
Simu +255 26 2321455, Faksi +255 26 2321457.
Barua pepe: info@rldc.co.tz.
Tovuti: www.rldc.co.tz.